

### 13-Al-Waqf Wal-Ibtidaai (Kisimamo Na Kianzio)

الْوَقْفُ وَالْإِبْتِدَاءُ

Tofauti baina ya **الْوَقْفُ Al-Waqf (Kisimamo)**, **السَّكْتُ As-Sakt (Kipumziko au Kinyamazo)** na **الْقَطْعُ Al-Qatw'u (Ukataji)**

Istilahi hizi tatu hutumika katika fani ya kusoma Qur-aan na kila moja ina maana na kusudio lake na pahala pake pa kutumia ijapokuwa zinaonyesha kama zote zina maana moja.

**الْوَقْفُ Al-Waqf - Kisimamo:**

Ni kukatika sauti katika neno la Qur-aan kwa muda wa kawaida ya mtu kushusha pumzi na huku akiwa na nia ya kuendelea katika kusoma.

**السَّكْتُ Al-Sakt - Kipumziko:**

Ni kipumziko katika kusoma neno la Qur-aan kadiri ya haraka mbili bila ya kushusha pumzi kwa nia ya kuendelea katika kusoma.

**الْقَطْعُ Al-Qatw'u Ukataji:**

Ni kusimama kusoma Qur-aan kwa nia ya kumaliza kuisoma, na haijuzu kusimama isipokuwa mwisho wa Aayah au mwisho wa Suwrah; na msomaji atapotaka kurejea kusoma Qur-aan kwa mara nyengine baada ya kukata, ni juu yake kuleta **الِإِسْتِعَاذَةَ** - Isti'aadhah.